

# Usajili biashara ndogo kupitia tovuti kitendawili

**Brela inapaswa kuweka utaratibu wa kisasa ili kuharakisha usajili wa biashara.**

Veneranda Sumila, Mwananchi

Shirikisho la wafanyabiashara ndogondogo nchini (Vibindo) linaamini kwamba sehemu kubwa ya biashara ndogo nchini zingekuwa rasmi, kama utaratibu wa kuzisajili ungekuwa rahisi na usiokuwa na bughudha.

Hayo yanatokana na ukweli kwamba sehemu kubwa ya biashara ndogo nchini hazijasajiliwa kutokana na kukosekana kwa utaratibu rahisi wa kusajili biashara hizo.

**Vigumu kusajili biashara**

Mwenyekiti wa Vibindo Gaston Kikuwi anasema wakati Rwanda inachukua saa moja kusajili biashara kwa tovuti, Tanzania inachukua siku moja hadi tatu.

"Pamoja na hayo mtu hawezi kumaliza usajili wake kwa njia ya tovuti, kwani itambidi azuru ofisi za usajili za Wakala wa Kusajili na Kutoa Leseni za Biashara (Brela) mwenyewe, akiwa Dar es Salaam au ofisi za Chama cha Wenye Viwanda, Biashara na Kilimo (TCCIA)," anasema Kikuwi.

Katika tovuti ya Brela, www.Brelatz.org, unachoweza kufanya ni kupata fomu za kuombea jina la biashara na kutafuta majina ya biashara ili muombaji apate jina atakalotumia. Kwa mfano, mwaka huu majina yaliyosajiliwa mwaka 2012 bado kuingizwa kwenye mtandao.

Kutokana na ukweli huo kazi ya kutafuta jina ni ngumu kwani wakati mwingine unaweza kuchukua jina ambalo lipo tayari ila halijaingizwa katika mfumo na kukataliwa wakati wa ukaguzi.

Kikuwi anasema pamoja na juhudi za Serikali kukabiliana na hali hiyo ipo haja ya hatua za makusudi kuchukuliwa ili wafanyabiashara wadogo wasione taabu kusajili biashara zao. Hatua hiyo ni pamoja na kuondoka na tozo katika usajili.

"Mwaka jana Serikali ilipendekeza kipitia Brela kwamba tozo ya usajili wa jina la biashara kuongezwa kutoka Sh5,000 hadi Sh50,000, wafanyabiashara wadogo hawakuridhika na baadae walikubaliana na wananchi tozo liwe Sh15,000," alisema Kikuwi

Mwenyekiti huyo anabainisha kwamba japokuwa serikali inafikiria kuongeza pato, ana wasiwasi kwamba kuongezwa kwa tozo hilo halitasaidia mapato ya Serikali.

"Ni vyema kama Serikali itaangalia namna nzuri ya kuongeza kipato chake kwa kuhakikisha kwamba inaweka mfidhawa ambao utahakikisha Watanzania wote wanalipa kodi kwa hiari," anasema Kikuwi.

Anasema usajili wa jina la biashara ni sehemu ya mfanyabiashara kutaka kutambuliwa, hivyo kuongeza gharama za huduma hiyo si sahihi watu wanaweza kukimbia na hili siyo jambo zuri kwa serikali hasa kwa kuzingatia kwamba biashara nyingi zinafanyika bila utambulisho.

Kwa mujibu wa Kikuwi tozo hizo za huduma zinaweza kuwa na athari mbaya kwa nia njema ya Serikali, kwani zinaweza kabisa kuwakimbiza wahusika.

Taarifa ya utafiti ya hivi karibuni ya Vibindo kuhusu suala la usajili na tozo inataka kiwango cha sasa kuendelea au kuongezwa kidogo.

"Serikali inapaswa kuangalia usajili wa wafanyabiashara wadogo kama sehemu ya kutaka kutambuliwa na wanapofanya hivyo inawajenga wao na kushawishi wengine kujitambua na kujisajili na mwisho kuongeza pato la taifa," inasema taarifa hiyo ya utafiti.

Utafiti huo wa Vibindo uliofanywa kwa udhamini wa BEST-AC umebainisha kwamba ongezeko la tozo la huduma limefanyika bila kuhusisha wadau wahusika katika hatua zake za awali.

"Ni msimamo wa wafanyabiashara wadogo katika sekta binafsi wakiongozwa na Vibindo kuwa suala la tozo katika huduma lifanyiwe kazi baada ya majadiliano mapana," inasema sehemu ya utafiti huo.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo ya utafiti wakati Tanzania inatoza Sh5,000 kwa kusajili jina la kampuni au biashara majirani zetu wa Rwanda hufanya hivyo kwa faranga 1,000 sawa na Sh 2,500.

"Hii inaonyesha kwamba Watanzania wao wanalipa zaidi kuliko majirani zao. Mapendekezo ya nyongeza yatafanya tofauti iwe kubwa zaidi," ilisema taarifa hiyo.

Kikuwi anasema mamia ya wafanyabiashara wadogo nchini ambao ambao wanajishughulisha na biashara mbalimbali, hawajasajiliwa na wamekuwa wakiendesha shughuli zao kimya kimya.

"Ongezeko kubwa katika tozo la usajili wa biashara na kurejeshwa kwa tozo ya leseni ya biashara kuongeza juhudi za kushawishi wengi zaidi watambulishe biashara zao," anasema Kikuwi.

Pamoja na kulipa tozo kubwa ya usajili, kwa mujibu wa Vibindo kuna gharama nyingine zilizojificha za usajili wa jina la biashara.

Huduma za Brela hupatikana Dar es Salaam pekee japo siku hizi juhudi zinafanyika kupunguza tatizo hilo hasa kwa kuzipa uwakala ofisi za TCCIA mikoani, lakini kwa nyongeza ya tozo.

**Kuna urasimu mkubwa**

Pamoja na maelezo matamu ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko kwa bajeti ya mwaka 2011/12 kwamba usajili wa biashara sasa unapaswa kufanywa kwa siku moja, wanasema kwamba hilo haliwezekani labda mfanyabiashara huyo awe Dar es salaam.

Hata akiwa Dar es Salaam mambo hayawezi kuwa rahisi hivyo.

"Wakala umezingwa na urasimu mkubwa, huduma zinazotolewa kizamani zaidi badala ya kutumiwa kwa tovuti halafu kumekuwapo na kusitasita kuweka mifumo itakayowezesha usajili kufanyika kwa njia ya tovuti moja kwa moja," imesema sehemu ya ripoti hiyo.

Kwa mujibu wa Kikuwi, wakazi wa nje ya Dar es Salaam, usajili wa biashara zao huchukua miezi kadhaa.

Anabainisha kwamba nchini Rwanda, mtu anaweza kukamilisha usajili wake kupitia tovuti kwa kipindi cha saa moja tu. Brela wanapaswa kujifunza kutoka Rwanda.

Vibindo imesema katika utafiti wake kwamba tozo hizo za usajili zisitumike kama pato kwa Wakala na badala yake Brela wangelifanya kila linalowezekana kushawishi watu wengi zaidi wasajili biashara zao.

**Tujadiliane kupitia Ujumbe mfupi SMS kwa 15774 ukianza na neno BIZ na kufuatia ujumbe wako. Ujumbe wako mfupi ni bure, hautozwi.**

Machungwa ni baadhi ya bidhaa ambazo zinapaswa kusajiliwa Brella, lakini wengi hawafanyi hivyo. **Picha na Maktaba.**

## TAARIFA ZAIDI



- Serikali inapaswa kuangalia usajili wa wafanyabiashara wadogo kama sehemu ya kutaka kutambuliwa na wanapofanya hivyo inawajenga.
- Huduma za kusajili kampuni zinapatikana Dar es Salaam tu.
- Serikali kwa kushirikiana na Brella iweke nguvu kusajili biashara ndogo na kubwa ili ikusanye mapato mengi zaidi.

BEST-AC
Tuboreshe mazingira ya biashara
Doing business, let's make it easy
UKURASA HUU UNADHAMINIWA NA BEST-AC NA MWANANCHI